
# MPANGO WA UWEZESHAJI WA FEDHA









Wapiga picha:
Jacqueline Namfua & Rob Beechey

UNCDF

# Kufungua Fursa za Kifedha kwa Umma na Sekta Binafsi kwa ajili ya Wajasiriamali wadogo

Kuimarisha uwezo wa Serikali za Mitaa na ushirikishwaji wa sekta binafsi. Kujenga taasisi zenye ufanisi kwa ajili ya fedha za umma na binafsi.

Mtiririko wa mtaji kwenye taasisi za ngazi ya mahalia kwa ajili ya fedha za umma na binafsi.

Kusimamia matokeo ya kimabadiliko.

Siyo kweli kwamba hakuna ujasiriamali nchini Tanzania, kinachofanya ndoto nyingi zisitimie ni ukosefu wa fursa za mitaji kwa ajili ya miradi ya maendeleo nchini na mlolongo wa michakato inayohitajika ili kubadili ndoto na mawazo ya kijasiriamali kuweza kutekelezwa katika uhalisia.

Umuhimu wa uwekezaji katika uchumi wa nchi zinazoendelea ni suala linalofahamika vema, lakini viwango vya sasa viko chini mno – hususan katika uchumi wa mahalia – na masoko ya fedha bado hayajakomaa vya kutosha.


Programu ya Fedha za Mahalia (LFI) ni programu pekee ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Mitaji (UNCDF) inayofanya kazi kubwa kondoa vikwazo hivi. LFI hutumia utaratibu wa kutoa kianzio cha mtaji wa uwekezaji na msaada wa kiutaalam kwa kulenga kupunguza hatari inayoweza kuwakabili wawekezaji binafsi, kama vile benki, katika kuwekeza fedha kwenye miundombinu muhimu ya kiuchumi na huduma za msingi katika ngazi ya jamii.

## LFI Tanzania

LFI Tanzania (LFI-T) husaidia wajasiriamali wote kutoka sekta ya umma na sekta binafsi katika kuandaa na kutengeneza miradi ya uwekezaji inayotekelezeka na yenye kustahili kukopeshwa na kuonyesha namna miradi hiyo inavyoweza kuzaa matunda kiuchumi na kijamii. Uwekezaji uliobuniwa vizuri katika kiwango cha chini cha uwekezaji– mfano, usindikaji mazao ya kilimo, nishati ya umeme vijijini utokanao na vyanzo vya maji, stendi za mabasi na masoko kwa ajili ya huduma za jamii, na miundombinu ya mawasiliano – yote yanaleta mabadiliko chanya katika jamii kote nchini Tanzania, kwa kusaidia usalama wa chakula, kuwezesha wanawake na vijana, kutengeneza fursa za ajira, mabadiliko ya tabia ya nchi na vyanzo vya nishati salama.


Katika msingi wake, LFI inalenga kuhakikisha kuwa watu katika mikoa na maeneo yote wananufaika kutokana na kuchangia katika maendeleo ya taifa. Kuwekeza mitaji katika rasilimali za ndani hapa nchini husaidia kupandisha thamani ya bidhaa za ndani na kujenga uchumi imara wa mahalia ulio jumuishi, wenye kuzalisha na wenye uwezo wa kujinusuru na hivyo kuwa wenye uchangiaji motomoto katika ukuaji. Kwa kuongezea, kazi yetu na mamlaka za serikali za mitaa inalenga kuimarisha uwezo wao wa kuanzisha miradi kama hiyo kama sehemu ya kutekeleza mipango yao ya kibajeti ya kila mwaka kwa upande wauwekezaji. Matokeo yake ni kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kupata vyanzo vya mitaji kutoka katika sekta binafsi na masoko ya mitaji ya mahalia na kuongeza mapato kwa kutoa huduma bora kwa umma. Matokeo mengine muhimu ni uchumi wa mahalia ulio imara na mamlaka za serikali za mitaa zinazojitosheleza ambazo hazitegemei sana serikali kuu katika masuala ya rasilimali fedha.

## Njia na Mtiririko wa Mchakato wa LFI



Tangu kuzinduliwa kwake mwaka 2012, LFI-T imesaidia zaidi ya miradi 30 ya maendeleo nchini Tanzania kutoka hatua za ubunifu wa miradi hadi hatua ya kuwa tayari kwa uwekezaji, kwa kufanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na taasisi za fedha. LFI-T inasaidia miradi katika mikoa 18, iliyotawanyika katika sekta mbalimbali – usalama au utoshelevu wa chakula; ustahimilivu wa mabadiliko ya hali ya tabianchi; nishati salama; uwezeshaji wanawake kiuchumi na maendeleo ya ndani ya kiuchumi ikiwemo kuboresha miundo mbinu ya utoaji huduma za kijamii. Baadhi ya mifano ya kazi hii imeelezwa hapa chini.

## Sehemu ilipo miradi: Mgawanyiko wa miradi kisekta na kwa maeneo




**Usambazaji Umeme Vijijini/Nishati Salama:** Waanzilishi miradi watano kutoka sekta binafsi wanaendeleza miradi midogo midogo ya kuzalisha umeme wa maji (katika mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya) ili kuboresha upatikanaji umeme kwa biashara, kwenye vituo vya afya, shuleni na majumbani. Miongoni mwa manufaa makubwa ni kuleta umeme wa gharama nafuu na nishati ya kuaminika zaidi kwa biashara ndogondogo, kuokoa muda ambao wanawake na watoto waliutumia kutafuta kuni na pia kuwezesha kuhifadhi chakula kwenye jokofu. Miradi hiyo pia itawezesha kutengeneza mazingira safi na salama zaidi kwa kupunguza ufyekaji misitu na matumizi ya mkaa kwa ajili ya kupikia. LFI-T ilitoa kianzio mtaji na ushauri wa kiufundi ili kufanya miradi hiyo ikopesheke kupitia benki na kuwa tayari kwa uwekezaji. Kama matokeo ya msaada huo, miradi hii imepata ufadhili wa ziada kutoka Wakala wa Umeme Vijijini nchini Tanzania (REA), vifaa vya umeme wa maji kutoka katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuendeleza Viwanda (UNIDO) na ahadi ya mkopo kutoka katika benki ya kibiashara.

**Kilimo:** Chama cha Ushirika cha Kilimo cha Korosho (TANECU) kinataka kujenga kiwanda cha kubangua korosho mjini Mtwara ili kuwepo na soko la kuaminika kwa wanachama wake – wote wakiwa ni wakulima wadogowadogo, hasa wanawake ambayo italeta ongezeko la uzalishaji mali na kipato. Mradi huo pia utatengeneza ajira mpya, utachangia katika kufufua uchumi wa vijijiji na kuongeza nguvu ya kipato cha fedha za kigeni. LFI-T inatoa ushauri wa kiutaalam na kianzio cha mtaji, fedha za mtaji zaidi zinatarajiwa kutolewa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Benki ya Maendeleo ya TIB.

**Utoaji Huduma za Jamii:** Serikali nyingi za mitaa zinataka kujenga miundombinu ya uchumi ili kutoa huduma bora za jamii katika maeneo yao, lakini mara nyingi zinalazimika kusubiri fedha isiyotosheleza kutoka serikali kuu. LFI-T huzisaidia serikali za mitaa kufikia malengo yao kwa kutumia mtaji binafsi. Halmashauri ya Mji wa Kibaha (Mkoa wa Pwani) imepata msaada wa kiutaalam kutoka LFI-T na wengineo ili kujenga soko na tendi ya mabasi ya kisasa ili kuwahudumia wananchi na abiria wapatao 60,000 kila siku; kuwapa wakulima na wafanyabiashara wadogo (hasa wanawake) fursa ya kupata soko safi, lililojengwa vizuri na la pamoja kwa ajili ya mazao yao ya kilimo, na hivyo kutoa fursa ya kuanzishwa kwa biashara ndogondogo. LFI-T ilishirikiana kwa karibu na Halmashauri ya Mji ili kutengeneza vizuri miradi yake ili iweze kukidhi viwango vya kibenki vya ukopeshaji, na zaidi ya hayo ilitoa mtaji wa kuanzia kama sehemu ya mtaji ili kufanya mkopo uwezekane. Matokeo yake, Benki ya Maendeleo ya TIB ilikubali kutoa mikopo inayotosha kugharimia robo tatu ya gharama za miradi yote miwili. Kodi, ushuru na ada zitakazoongezeka kutoka katika miradi hii ndivyo vitaiwezesha Halmashauri ya Mji kulipa mikopo hiyo.

# Kisa Mafunzo cha LFI: Soko la kisasa la Kibaha



## Maelezo ya Mradi:

- Sekta: Miundombinu ya utoaji huduma za jamii
- Mradi: Soko la kisasa
- Mahali: Mji wa Kibaha, Mkoa wa Pwani
- Gharama: $10.1 milioni; mkopo wa benki $7.6 milioni
- Mchango wa UNCDF: Kianzio mtaji $252,160 na msaada wa kiutaalam



Soko la sasa pale Maili Moja, Kibaha



Soko la kisasa linalopendekezwa

Jumla ya gharama ya mradi wa soko la kisasa la Kibaha ni karibu dola za Marekani milioni 10.1. LFI ilitoa ushauri wa kiutaalam  ili kuthibitisha kuwa suala hilo linawezekana kibiashara na kianzio mtaji cha dola za Marekani 252,160 ili kuziba pengo katika mchango wa mtaji wa mradi kwa Halmashauri ya Mji wa Kibaha. Mchango huu, ukiongeza na ule wa wengine, utafungulia mtaji kutoka nchini, ikiwa ni pamoja na mkopo wa dola za Marekani milioni 7.6, sawasawa na robo tatu ya gharama ya jumla ya uwekezaji kutoka katika Benki ya Rasilimali ya Tanzania.

*"Hatuna soko, tumekuwa na magenge tu katika mji wetu huu wa Kibaha. Pia tuna kituo kidogo cha mabasi ambacho hakitoshelezi mahitaji ya usafiri kwa wakazi wa Kibaha – hii imekua changamoto yetu kubwa katika kipindi cha zaidi ya miaka kumi sasa. Mji wetu unakua na sasa tunahitaji huduma bora na za kisasa. Makubaliano ya mkopo kutoka Benki ya Rasilimali ya Tanzania ni matokeo makubwa ya msaada wa kiutaalamu ambao tumekuwa tukipewa na UNCDF, hasa wakati wa kuongea na benki pale ambapo halmashauri ilikuwa ina changamoto.  Kila wakati tulipokuwa na mkutano na benki walikuwa pamoja nasi kuhakikisha tunakuwa na majadiliano ya mafanikio. Kiujumla, tunawashukuru UNCDF kwa msaada waliotupatia. Halmashauri ya Mji wa Kibaha inamajukumu ya kutoa huduma kwa jamii na hili soko la kisasa litasaidia kuongeza mapato ya Kibaha."*

Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya mji wa Kibaha. – Ms. Jenifa Omolo.

LFI-T itaendelea kufanya kazi nchini Tanzania hadi mwaka 2019. Serikali ya Tanzania tayari imeonyesha nia ya kutumia mbinu na mikakati ya LFI katika mamlaka zote za serikali za mitaa nchini. Programu ya LFI pia ilizinduliwa nchini Uganda mwezi Oktoba 2015 na Benin mwezi Novemba 2015.

**Mfuko wa Maendeleo ya Mitaji wa Umoja wa Mataifa**
Kitalu namba 421, mtaa wa Mahando, Masaki
Namba ya simu: +255 737217574
Barua pepe: local.finance@uncdf.org
Tovuti: www.uncdf.org
Facebook: UNCDFLFI
Twitter: @UNCDFLFI

UNCDF